# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

## MWELEKEO WA MVUA TANZANIA
## KATIKA KIPINDI CHA JANUARI – MACHI, 2019

**Dondoo muhimu za mvua kwa kipindi cha Januari-Machi, 2019**

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa mvua katika kipindi cha **Januari-Machi, 2019**. Kwa muhtasari, mwelekeo huo unaonesha kuwa:

a) **Mwelekeo wa mvua katika kipindi cha Januari-Machi, 2019:**

- Vipindi vya mvua za nje ya msimu vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Kanda ya Ziwa Victoria, Nyanda za juu kaskazini Mashariki, Pwani ya kaskazini pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma) hususani katika mwezi Januari, 2019
- Mvua zinazoendelea katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa, Mtwara na Lindi; pamoja na maeneo yaliyopo kusini mwa mkoa wa Morogoro. Aidha, mikoa ya Tabora, Katavi, Kigoma, Rukwa, Dodoma, Singida, Njombe na Ruvuma inatarajiwa kupata mvua za wastani.
- Kuna uwezekano wa kutokea vimbunga katika bahari ya Hindi ambavyo vinatarajiwa kuathiri (kuongeza au kupunguza) mvua katika baadhi ya maeneo nchini.

## 1. MWELEKEO WA MVUA KWA KIPINDI CHA JANUARI – MACHI 2019.

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa (Kama ilivyoelezwa katika kipengele 2 cha taarifa hii), kuna uwezekano mkubwa wa mvua za wastani katika maeneo mengi nchini. Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo ni kama ifuatavyo:

### 1.1. Mvua za Msimu:

Mvua za Msimu ambazo zilianza mwezi Novemba, 2018 zinatarajiwa kuendelea vizuri katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua. Kwa ujumla mvua hizi zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa, Mtwara, Lindi pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro. Kwa upande mwingine mikoa ya Tabora, Katavi, Kigoma, Rukwa, Dodoma, Singida, Njombe na Ruvuma inatarajiwa kupata mvua za wastani.

Vipindi vya ukavu vinatarajiwa hususani katika mwezi Februari, 2019, na mwezi Machi mvua zinatarajiwa kuendelea.

#### 1.1.1 Kanda ya Magharibi: (Mikoa ya Tabora, Rukwa, Katavi na Kigoma):

Katika kipindi cha JFM, 2019, mvua za wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Katavi na Rukwa.

#### 1.1.2 Kanda ya Kati (Mikoa ya Singida na Dodoma):

Katika kipindi cha JFM, 2019 maeneo ya kati mwa nchi yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo machache. Maeneo mengi yanatarajiwa kuwa na mvua za wastani kwa ujumla.

#### 1.1.3 Nyanda za juu kusini magharibi pamoja na maeneo ya kusini mwa nchi: (Mikoa ya Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe na Ruvuma; pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro):

Mvua za wastani hadi juu ya wastani kwa ujumla zinatarajiwa katika kipindi cha JFM, 2019 kwa maeneo ya Nyanda za juu kusini magharibi; Maeneo ya kusini mwa nchi yanatarajiwa kupata mvua za wastani.

**1.1.4 Pwani ya Kusini: (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Kwa ujumla mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika kipindi cha JFM, 2019. Aidha, upo uwezekano wa kupata ongezeko la mvua kuanzia wiki ya nne ya mwezi Februari, 2019.

**1.2 Mvua za msimu wa '*Vuli*'**

Mvua za *'Vuli'* kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua (Kanda ya Ziwa Victoria, Nyanda za juu kaskazini mashariki, Pwani ya kaskazini pamoja na Wilaya ya Kibondo) zimeisha mwezi Disemba, 2018. Hata hivyo, mvua za nje ya msimu zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususani katika mwezi Januari, 2019. Kwa ujumla hali ya ukavu inatarajiwa katika kipindi cha mwezi Februari, 2019.

**1.2.1 Kanda ya Ziwa Victoria: (Mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Geita, Simiyu na Shinyanga):**

Mvua za nje ya msimu zinatarajiwa hususani katika mwezi Januari, 2019 na zinatarajiwa kuwa za wastani.

**1.2.2 Ukanda wa Pwani ya Kaskazini: (Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Pwani, Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Morogoro):**

Mvua za nje ya msimu zinatarajiwa hususani katika mwezi Januari, 2019 na zinatarajiwa kuwa za wastani.

**1.2.3 Nyanda za juu Kaskazini Mashariki: (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Mvua za nje ya msimu zinatarajiwa katika mwezi Januari, 2019. Hata hivyo, kuna uwezekano wa mvua hizo kuongezeka katika baadhi ya maeneo hususani kati ya wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Januari, 2019. Kwa ujumla mvua hizi zinatarajiwa kuwa za wastani.

## 2. MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la juu ya wastani iliyopo katikati mwa eneo la Kiikweta la Bahari ya Pasifiki (CEPO) pamoja na kusini magharibi mwa bahari ya Hindi (SWIO) inatarajiwa kuendelea kuwepo katika kipindi cha Januari-Machi, 2019. Hali ya joto la juu ya wastani inatarajiwa magharibi pamoja na maeneo ya kati mwa bahari ya Hindi, kwa upande mwingine, hali ya joto la wastani hadi chini ya wastani inatarajiwa mashariki mwa bahari ya Hindi (EIO). Joto la bahari la juu ya wastani upande wa magharibi mwa bahari ya Hindi (SWIO) pamoja na joto la chini ya wastani mashariki mwa bahari ya Hindi (EIO) linatarajiwa kuongeza uwepo wa upepo wenye unyevunyevu kutoka mashariki kuelekea katika Pwani ya nchi hususani katika mwezi Machi, 2019. Hali ya joto la juu ya wastani mashariki mwa kisiwa cha Madagascar inaashiria kuwepo kwa uwezekano mkubwa wa migandamizo midogo ya hali ya hewa inayowezesha vimbunga kujitengeneza katika eneo hilo. Aidha, hali ya joto la chini ya wastani linalotarajiwa katika eneo la pwani ya Angola, inatarajiwa kuchangia kuwepo kwa upepo wenye unyevunyevu kutoka magharibi katika misitu ya Kongo na hivyo kuongeza mvua katika baadhi ya maeneo hapa nchini.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

***Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo utazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia tabiri za saa 24, siku 10 pamoja na za mwezi kama zinavyotolewa na Mamlaka ya hali ya Hewa Tanzania.***

Mamlaka ya hali ya hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa taarifa za mwelekeo wa mvua nchini.

Imetolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania:

Dkt. Agnes L. Kijazi

**Mkurugenzi Mkuu**